

**Dondoo za mukutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam**  
**3 Januari 2009**

**Waliohudhuria**

Bashiri Rashidi  
Elaine Baker  
Filbert Mbecha  
Hamadi Hatibu Bwaja  
Juma Ali Salehe Jongo  
Juma Hassan Chibaya  
Jumanne Ayuba  
Kibwana Mohammad Msiga  
Mohammed Samwely  
Paulo Atibu Hatibu  
Shamte J Kigoma  
Solomon Mihoyo  
Sudi Saidi Ramadhan

**Volunteer**

Bado hatujapata mawasiliano kutoka Johannes au TASEA na hatujaweza kuwapata kwa simu na hatujapata jibu la email. Tutaendelea kujaribu.

**Repoti ya msafara**

Elaine atampa Mejah nakala ya repoti ili kupeleka kwa Business Times.

**Mradi wa Wamba**

Dr Una Osili alijibu email na alisema wataangalia jinsi ya kututumia fedha zinazobaki. Tutatumia email nyingine ili kufuatalia.

**Video ya usalama wa baiskeli**

Elaine hajaweka video kwenye DVD wiki hii tena atafanya.

**Kalenda**

Huu ni mukutano wa kwanza wa 2009. Tulikubali kuomba kalenda kutoka Chuo cha Usafirishaji NIT National Institute of Transport kuweka ofisini kwetu.

**Mpango wa mukutano na serekali ya jiji na kongamano**

Filbert alienda kufuatalia barua yetu kuomba mukutano na serekali ya jiji. Aliongea na mwanamume ambaye ni ofisa kwenye idara ya mipanga lakini hajapata jina lake. Ofisa aliuliza maswali kuhusu UWABA na Filbert alieleza kuhusu miradi yetu kama elimu ya usalama wa baiskeli na mawasiliano na TANROADS. Ofisa alisema itakuwa nzuri kutana idara yake na UWABA. Alisema watajibu barua yetu na watatupa appointment.

### **Foundation for Civil Society**

Elaine alipata taarifa kutoka University Computing Centre kwamba wanaweza kufanya kozi ya kompyuta kwa wanachama wetu 20 kwa jioni tatu kila wiki kwa masaa mawili kila mara kwa miezi mitatu kwa gharama ya Tsh 120,000 kwa mtu ambayo ni Tsh 2,400,000. Tulienda Argentina Internet café kupata taarifa kuhusu kupata nafasi ya kutumia kompyuta yao kufanya mazoezi lakini menaja hakuwepo lakini tulipata namba ya simu yake. Elaine atauliza British Council kuhusu kozi ya kiingereza.

### **Wizara ya Miundombinu**

Idrisi hakuwepo katuambia kama amepeleka barua. Elaine ataleta nakala nyingine ili mtu mwengine afanye kazi hiyo.

### **NSSF**

Mejah alimwambia Hamadi kwamba amefuatalia kuhusu barua ya NSSF lakini hatuna taarifa nyingine.

### **Service Roads**

TANROADS Dar es Salaam wameweka alama Morogoro Road maeneo ya Manzese Darajani zinazosema ni marufuku kwa magari kuendesha wala kupaki kwenye sehemu ya hifadhi ya barabara. Kiasi ya magari yanayofanya hivi kwenye eneo hili imepungua lakini bado kuna magari mengi wanaendesha na kupaki maeneo mengine ya service road. Tulikubali kuandika barua kwa TANROADS kuwapongeza na pia kuomba waweke alama kwenye maeneo mengine.

### **Hela na guta**

Ally Saidi Mwishehe alitumia Tsh 14,000 ya hela ya guta kwa kupitia Filbert. Juma alitumia Tsh 1,500 kwa pini za bao ya tangazo. Juma sasa ana Tsh 40,800 ya hela ya UWABA. Juma alisema bado Tsh 14,000 ya hela ya guta inadaiwa.

### **Mambo mengine**

Filbert alisikia kwenye taarifa ya habari kwamba Corporal Abu, traffic police ambaye alishirikiana na UWABA, alijehuriwa kwenye ajali ya barabara Kibaha. Tulikubali kutafuta taarifa amelazwa wapi ili tumtembelee.

Frank Peter alikuwa na umwa mbay ya malaria. Wanachama tulikubali kumtembelea

.